

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
SHULE YA SEKONDARI MALANGALI S.L.P 4, MALANGALI.

VISION : *Malangali Secondary School is Determined to Enhance Students' Potentiality by Becoming Knowledgeable Skilfull and Professional to Foster Development Economically,Socially,Culturally and Technologically in Tanzania and World at Large.*

MISSION : *To enable Students to Excel in Academic.*

MOTTO : *Never Give In.*

Kumb. Na. U. 19/Vol.V.II/ 220

Ndg
.....
.....

YAH: MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA
MWAKA 2022

Ninayo furaha kubwa kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule hii. Nakupongeza sana kwa kuchaguliwa na nategemea utaitumia nafasi hii ipasavyo ili kujenga historia nzuri ya maisha yako. Ni mategemeo ya shule kuwa uwapo hapa utashirikiana vizuri na walimu, Watumishi wasio walimu na wanafunzi wenzako kufanya kazi za darasani na nje ya darasa. Unatakiwa kufika shuleni tarehe **11/01/2022.** ili kuanza masomo yako kikamilifu na kwa wakati. Ukichelewa utaipoteza nafasi hii adimu.

MAHALI SHULE ILIPO NA NAMNA YA KUFIKA SHULENI

Shule ipo Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Mufindi, Tarafa ya Malangali na Kata ya Malangali. Ukitokea Mafinga au Makambako kwa kufuata barabara kuu itokayo Dar es salaam kwenda Mbeya, Shukia kituo cha mabasi kiitwacho Mbalamaziwa, hapo utapata usafiri wa kuja Malangali sekondari umbali wa kilometa 18 Magharibi mwa mbalamaziwa.

3.0 SARE ZA SHULE

- 3.1 Shati mbili nyeupe kabisa tetron au Polista, zenye ukosi wa kawaida, mikono mifupi pamoja na tai mbili nyeusi na khaki.
- 3.2 Suruali ya khaki moja na nyeusi moja upana wa chini uwe wa inchi 18, iwe na rinda mbili kila upande na mifuko mitatu, mkanda wa kuvalia suruali uwe wa ngozi s rangi nyeusi (chuma cha kwenye mkanda kisiwe na urembo na maandishi ya aina yoyote, pia usiwe utambi).
- 3.3 Viatu vyeusi jozi mbili, visiwe buti, viwe vya kamba. Viatu visivyofungwa na kamba havikubaliki/haviruhusiwi.
- 3.4 Jozi mbili za soksi nyeusi
- 3.5 Fulana moja ya kijivu (T- shirt) huvaliwa siku ya Ijumaa zinapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/=, Sweta nadhifu la bluu lenye V shingoni, track suti nyeusi yenye mikanda ya rangi nyeupe mikononi, Raba au viatu vyeupe kwa ajili ya michezo. Jezi ya michezo rangi nyeusi (Bukta na Tshirt)
- 3.6 Shati moja rangi ya bluu bahari na suruali moja (rangi ya dark blue) kwa ajili ya kuvaa baada ya vipindi vya darasani.

3 :7 Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuja shuleni na ngou za nyumbani tofauti na zilizoagiwa.

4.0 VIFAA VYA MALAZI

- 4.1 Blanketi 1, shuka mbili za rangi ya pinki na mto wenye foronya ya rangi ya pinki
- 4.2 Godoro lenye upana wa futi mbili na nusu. (Lishonewa cover ambayo ni water proof)
- 4.3 Chandarua (Mosquito net) kwa ajili ya kujikinga na malaria.
- 4.4 Trucker / sanduku la chuma la kuhifadhia vifaa vyako uwapo shuleni

6.0 VIFAA VYA CHAKULA

- 6.1 Kontena, Kikombe na Kijiko.

7.0 VIFAA VYA TAALUMA

- 7.1 Mnunulie mtoto vitabu vya masomo ya Hisabati, Fizikia, Elimu ya viumbe, Kiswahili, Kiingereza, Historia, Jiografia, Uraia na Kifaransa kwaajili ya matumizi yake. Shule ina vitabu

lakini havitoshelezi kwa kila mwanafunzi.

- 7.2 Uje na daftari kubwa (Counter books) zisizopungua 12, mathematical set na peni za kutosha.
- 7.3 **Spring file 2**, moja ndani yake kuwe na kivuli cha cheti cha kuzaliwa, fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule, hati ya mganga iliyojazwa baada ya kupimwa.
- 7.4 Uje na karatasi bando mbili A4 (Ream Paper 2)

8.0 AFYA

- 8.1 Uje na ndoo mbili zenye mifuniko na mfagio wa chelewa kwa usafi binafsi, vyoo vyetu ni vile vya maji na maji eneo hili siyo ya kutosha. Pia uje na toilet paper 05
- 8.2 Aidha matibabu ni juu ya mzazi/mlezi na fedha kwaajili ya matumizi yake binafsi.
- 8.3 **Ni vema akaja na kadi ya Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu.**
- 8.4. Kwa ajili ya kujikinga na magonjwa ya ngozi miguuni na sehemu za siri aje na taulo na nguo za ndani za kutosha.

9.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

- 9.1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978.
Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini.
Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

- (a) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule ndani na nje ya shule ni muhimu
- (b) Kutimiza kwa makini maandalio ya siku (Preparation) na siku za mwisho wa wiki.
- (c) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- (f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (h) **MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUMILIKI AU KUTUMIA SIMU KIPINDI CHOTE AWAPO SHULENI.**

9.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZA SHULENI.

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga
3. Ulevi na matumizi mabaya ya madawa ya kulevywa. kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli nakadhalika.
4. Uvutaji bangi na sigara
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoja/kusababisha mimba
10. Kulawiti
11. Utoro

12. Kutofanya mazoezi au mitihani ya masomo na kutega vipindi
13. Kiburi na ukaidi
14. Kugoma/kuchochea na kuongoza mgomo
15. Kukataa adhabu kwa makusudi
16. Kumiliki/kutumia simu shuleni
17. Kuchelewa kufika shuleni baada ya shule kufungua na kutoroka kabla ya shule kufungwa

10.0 Tumia tovuti hii kwa maelezo zaidi www.malangaliboyshighschool.com

TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAAGIZO HAYA NA KUYATEKELEZA UTAPOKELEWA SHULENI BAADA YA KUTIMIZA YOTE ULIOAGIZWA. NAKUTAKIA SAFARI NJEMA, KARIBU SANA MALANGALI.

.....
AMAN J. NYAHI (0763 401 829) / (0737365672)
MKUU WA SHULE

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT MUFINDI
DISRICT COUNCIL MALANGALI SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by medical officers in a recognized Hospital in respect of all new entrants of Malangali Secondary School

Full Name.....

Age.....

1. Blood comment (red & white).....

3. Urine examination.....

4. Stool examination.....

5. Syphilis test.....

6. T.B. test.....

7. Ear test.....

8. Spleen.....

9. Abdominal

10. Eye test.....

11. Additional information or any other physical, hereditary or infectious diseases

.....
.....
.....

Treatment after examination

.....
.....
.....

MEDICAL CERTIFICATE

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue for further education

Signature.....

Designation.....

Station.....

Official stamp.....

Date.....


N.B Fomu hii ijazwe na Mganga katika Hospitali inayotambulika na serikali.

KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI

A. MWANAFUNZI NA MZAZI/ MLEZI

- i. Jina la mwanafunzi.....
- ii. Tarehe ya kuzaliwa.....mahali.....


- iii. Jina la Baba.....yu hai/ amefariki.....
- iv. Mahali anakoishi; kijiji/mji.....kata.....tarafa.....
- v. Kazi ya Baba
- vi. Anuani yake.....simu



- vii. Jina la Mama.....
- viii. Kazi ya Mama.....
- ix. Anuani yake.....simu.....
- x. Mahali anapoishi; kijiji/Mji.....kata.....tarafa.....



- xi. Jina la mlezi 01.....
- xii. Kazi yake.....
- xiii. Mahali anapoishi; kijiji/ Mji.....kata.....tarafa.....
- xiv. Anuani yake.....simu.....



- Jina la mlezi 02.....
- Kazi yake.....
- Mahali anapoishi; kijiji/ Mji.....kata.....tarafa.....
- Anuani yake.....simu.....



B. AHADI YA KUFUATA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE (MWANAFUNZI)

Mimi.....
Naahidi kufuata sheria,kanuni na taratibu za shule hii na kutekeleza maagizo yote yatakayotolewa na uongozi wa shule wakati wote nitakaokuwa ndani na nje ya shule. Sitajihusisha na migomo, fujo, wala makosa ya jinai.
Saini.....Tarehe.....

C. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimiambaye ni
Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi aliyeweka ahadi hapo juu, naahidi kumpatia ada ya shule, michango na mahitaji yote yanayotakiwa kujiunga na shule hii.
Saini.....Tarehe.....

SCHOOL SONG

- 1.) Malangali our,our school; (we are proud of you(x2))
Malangali; in academics you are first in the front line. x2

CHORUS

Our motto Malangali,
Never (x 3) given in Malangali,
Never (x 3) give up Malangali,
We are spiritually one,
We are happy.

- 2.) Never give in, in culture, gathering defenses,
Educate the people; Malangali,
To teach morals to the people this is your task.
- 3.) 16th of April 1928, this is your beginning,
This is your foundation, Malangali.
We are very happy, we thank you Malangali our school.
- 4.) Our lives' future, is in your hands, protect it from AIDS,
Protect it from danger, Malangali
So that we enjoy your fruits Malangali our school. x2

END

NB:

- [1] The first and fourth stanzas should be sung twice.
- [2] The chorus should be sung once for the first three stanzas. For the Last stanza Chorus should be sung twice.
- [3] The song leader introduces the song. He is the first to begin the first Stanza and the chorus.

